Mwananchi, Tarehe 26/11/2020 uk. 16

MASOKO

# Teknolojia ya kisasa kuondoa uvuvi wa kubahatisha baharini

Mwandishi Wetu, Mwananchi
makala@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Wakati Rais John Magufuli akipanga kujenga bandari ya uvuvi itakayoajiri watu 30,000, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imesema imekamilisha ujenzi wa maabara yenye uwezo wa kutambua mahali walipo samaki wa kutosha ili kuondokana na uvuvi wa kubahatisha.

Ujenzi wa maabara hiyo ni utekelezaji wa mradi wa miaka sita wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (*Swiofish*) unaotekelezwa katika wilaya za Mkinga, Tanga Jiji, Pangani, Bagamoyo na Lindi Vijijini tangu Juni 2015.

Mratibu wa mradi huo, Dk Nichrous Mlalila amesema maabara hiyo inasimamiwa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (Tafiri) kituo cha Kunduchi.

"Maabara itasaidia kubaini walipo samaki na sensa ya chombo kuondokana na uvuvi wa kubahatisha. Mkondo ya mwezi huamua aina ya vyakula vinavyopatikana hivyo kuwavutia samaki. Maabara hii itasaidia kujua aina ya samaki na wanapopatikana kwa wakati husika," amesema Dk Mlalila.

Licha ya kuwa na eneo mkubwa, maziwa na bahari bado Tanzania haijitosheleza kwa mahitaji ya samaki wala kunufaika sana na sekta ya uvuvi kutokana na uvuvi kufanywa kwa kubahatisha jambo ambalo sasa limepata mwarobaini.

Dk Mlalila amesema maabara hiyo ilikuwa ikabidhiwe Februari lakini kutokana na sababu kadhaa zilizojitokeza, itakabidhiwa Desemba na kuanza kufanya kazi mara moja.

Akizungumza akizindua Bunge la 12, Rais Magufuli alisema uvuvi katika bahari kuu unaweza kuingizia Taifa zaidi ya Sh352.1 bilioni kwa mwaka hivyo kwa kushirikiana na Shirika [illegible] Serikali itanunua meli nane na kujenga bandari kubwa ya uvuvi itakayotumika [illegible] nje kutoka nanga.

Ili kuwashirikisha wananchi wenye sekta hiyo, kuanzia Februari mwakani, wizara inakusudia kuliboresha Soko la Samaki Feri ambalo ni muhimu kwa wafanyabiashara wa samaki wa baharini jijini hapa ambalo linaonekana kuelemewa.

Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi, Ezra Mutagwaba amesema maandalizi yamekamilika. "Soko la Feri lilijengwa kuhudumia kati ya watu 1,500 mpaka 2,000 lakini kwa sasa kuna zaidi ya watu 15,000. Soko limeelemewa, miundombinu yake inahitaji kuboreshwa," amesema Mutagwaba.

Kuhusu mchakato mzima amesema wizara inamtafuta mkandarasi na "kwa sasa tunazungumza na mshauri elekezi, mpaka Januari tutakuwa tumempata na ujenzi utaanza mara moja."



**Sh352.1bil**

Mapato ambayo Serikali inaweza kuingiza kwa kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu

Scanned with CamScanner

The Guardian, Tarehe 26/11/2020 Uk.5

# * World Bank-funded project to renovate Dar fish market

By Guardian Reporter

THE World Bank-funded South-West Indian Ocean fisheries governance and shared growth project (SWIOFish) is set to refurbish the Dar es Salaam's Ferry Fish Market so as to cope with the increasing population and standards.

The market was designed to accommodate between 1,500 and 3,000 fishers, traders and customers, but the number has skyrocketed to over 12,000 people–four times the estimated number.

The market refurbishment is part of the implementation of the six-year project, which is aimed at improving the management effectiveness of selected priority fisheries at the regional, national and community level.

The project is implemented jointly by mainland Tanzania's ministry of Livestock and Fisheries (MLF), Zanzibar's Ministry of Agriculture, Natural Resources, Livestock and Fisheries and Deep Sea Fishing Authority (DSFA).

Despite its importance, Ferry Fish Market is in an appalling situation, whereby some of the market infrastructure–drainage system fails to accommodate waste generated at the facility.

"That's why SWIOFish project came up with the idea of revamping the market so that it remains with the same status," said Ezra Mutagwaba, acting director of fisheries in the ministry of Livestock and Fisheries.

"So far, a consultant is conducting a design study for the rehabilitation of Ferry Fish Market," said Dr Nichrous Mlalila, coordinator of SWIOFish when presenting a progress report of the project to the media practitioners in Dar es Salaam recently.

"The consultant has submitted the final design, environmental issues, environmental and social management plan (ESMP), and temporary relocation plan for the project to kick off," he said.

However, he said: "The World Bank demands comprehensive reports on and effects of reallocation of the communities working in the market, temporary reallocation plan."

> **"The ESMP and temporary relocation plan reports have been submitted to the WB waiting for approval**

Additionally, he said that the waste management systems were recommended to be improved in the design for approval.

"The ESMP and temporary relocation plan reports have been submitted to the WB waiting for approval," he said.

He also unveiled that through the project, a national mariculture resource centre at University of Dar es Salaam, Kunduchi Campus.

"The process to procure the consultant to design the centre failed for almost two years due to large tendered budgets above the allocated budget for the design."

He said: "The ministry requested the World Bank to change the budget cost from consultancy services to operational costs and to use the public expertise to design the centre." The World Bank recommended for memorandum of understanding and to establish control measures.

The ministry has formed a taskforce from public institutions which is led by Tanzania Building Agency (TBA) to design the centre.

The memorandum of understanding has been developed and submitted to the World Bank for no objection.

TBA has agreed to design and supervise in collaboration with other institutions.

Scanned with CamScanner

Mwananchi, Tarehe 26/11/2020 Uk. 2

# PICHA YA SIKU: HAPA SAWA

Mchuuzi akiwa amebeba samaki aina ya msusa baada ya kuwachukua kutoka kwa wavuvi waliotoka kuvua katika Bahari ya Hindi, akielekea kuwauza katika Soko la Deep Sea, jijini Tanga jana. **Picha na Filbert Rweyemamu**



Scanned with CamScanner